



## **TANGAZO LA KAZI KWA NAFASI YA FUNDI JUKWAA LA UJENZI**

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi, uendeshaji, na matengenezo ya bomba la kusafirisha mafuta ghafi kutoka Hoima Uganda mpaka Chongoleani Tanzania ambako kutajengwa gati na kituo cha kupakia mafuta ghafi karibu na bandari ya Tanga.

BESIX Ballast Nedam (BBN) Limited, ni MKANDARASI anayehusika kwenye mambo ya uhandisi, ununuzi na ujenzi wa gati na kituo cha kupakia mafuta ghafi ya mradi wa EACOP. BBN inawatangazia wazawa wa kata ya Chongoleani kuomba nafasi ya kazi ya Fundi Jukwaa la Ujenzi.

### **Nafasi za kazi – 2**

Mradi	EACOP – Jetty & Loading Out Facility
Muajiri	BESIX Ballast Nedam Limited (BBN)
Mahali pakazi	Tanga
Nafasi ya kazi	Fundi Jukwaa la Ujenzi
Mkuu wa Idara:	Meneja Ujenzi
Kipindi cha kazi	September 2023 – May 2025

### **Dhumuni la kazi**

Jukumu kuu la Fundi Jukwaa la Ujenzi ni kuunda na kufungua jukwaa la bomba za chuma katika majengo au maeneo ya ujenzi, ili watu wengine waweze kufanya kazi katika sehemu za juu kwa usalama. Fundi jukwaa anafunga jukwaa ndani ya jengo au katika maeneo ya nje ambako ujenzi, ukarabati au uvunjaji unafanyika.

### **Majukumu ya kazi**

- Kufunga jukwaa la ujenzi katika eneo la kazi.
- Kufungua jukwaa la ujenzi katika eneo la kazi.
- Kuhakikisha jukwaa limefungwa sehemu imara.
- Kufunga jukwaa kwenye majengo au maeneo mengine ya kazi.
- Kuweka sehemu za watu kusimama katika jukwaa.
- Kufunga nguzo/bomba pamoja na wavu wa usalama katika jukwaa.
- Kufunga aina mbalimbali za majukwaa ya ujenzi kadiri inavotakikana.
- Kuzingatia kanuni na tahadhari za usalama.
- Kazi nyingine zozote kadiri utavoelekezwa na kiongozi wako.

### **Sifa za muombaji.**

Muombaji awe na sifa zifuatazo:

- Elimu ya sekondari na mafunzo maalumu kwa uundaji jukwaa la ujenzi.
- Cheti cha mafunzo toka VETA ni muhimu.
- Uzoefu wa awali toka katika kampuni mashuhuri za ujenzi ni sifa ya ziada.
- Utimamu wa mwili na afya kwakuzingatia kazi inahitaji nguvu ili kubeba vifaa mbali mbali.



- Uwezo mzuri wa kuwasiliana na kufanya kazi kwa kushirikiana.
- Umakini wa kuzingatia tahadhari zote za usalama.

### **Vigezo na taratibu kwa waombaji**

- Awe raia wa Tanzania
- Umri kuanzia miaka kumi na nane (18) na kuendelea.
- Awe mzawa wa kata ya Chongoleani
- Asiwe na rekodi ya uhalifu
- Barua ya maombi ya kazi ikionyesha anuani pamoja na namba ya simu ya muombaji.

### **Jinsi ya kutuma maombi:**

Anuani kwaajili ya maombi ya kazi ni: **Meneja Mradi, BESIX Ballast Nedam Ltd. TANGA**. Maombi yote yatapokelewa kupitia ofisi ya kata ya Chongoleani au barua pepe [jobs@bbnltd.co.tz](mailto:jobs@bbnltd.co.tz) na mwisho wa kupokea maombi haya ni 10 Septemba 2023.

Majina ya watu wote watakaofanikiwa yatabandikwa katika mbao za matangazo kwenye ofisi ya mtaa husika.

**Kwa maswali/maelekezo;- +255 747 958 460** (ndani ya muda wa kazi, saa 1:00 asubuhi hadi saa 11:00 jioni, Jumatatu hadi Jumamosi)

**ZINGATIA.** Kwa nafasi hii, waombaji kutoka maeneo mengine ya Tanzania hawatakiwi kupiga muhuri barua zao za maombi katika Ofisi ya Kata ya Chongoleani, Ni wazawa wa kata ya Chongoleani wanaostahili kufanya hivyo.

**HAKUNA AJIRA MLANGONI!!! USITOE HELA KUPATA KAZI!!!**